**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

BODI YA SUKARI TANZANIA NA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA

# MWONGOZO WA USIMAMIZI WA BIASHARA YA ZAO LA MIWA YA SUKARI KUPITIA MFUMO WA VYAMA VYA USHIRIKA

**Mwongozo huu umetayarishwa na:**

Bodi ya Sukari Tanzania,
Barabara ya Sokoine/Mtaa wa Ohio,
S.L.P. 4355 Dar es Salaam - Tanzania.
Simu: +255 22 2111523,
Nukushi: +255 22 2130598.
Barua pepe: info@sbt.go.tz

Tume ya Maendeleo ya Ushirika,
Mtaa wa Kuu,
S. L. P 201 Dodoma – Tanzania.
Simu: +255 26 232 2993.
Barua pepe: ushirika@ushika.go.tz

*Toleo la Kwanza*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

BODI YA SUKARI TANZANIA NA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA

# MWONGOZO WA USIMAMIZI WA BIASHARA YA ZAO LA MIWA YA SUKARI KUPITIA MFUMO WA VYAMA VYA USHIRIKA

**Mwongozo huu umetayarishwa na:**


Bodi ya Sukari Tanzania,
Barabara ya Sokoine/Mtaa wa Ohio,
S.L.P. 4355 Dar es Salaam - Tanzania.
Simu: +255 22 2111523,
Nukushi: +255 22 2130598.
Barua pepe: info@sbt.go.tz

Tume ya Maendeleo ya Ushirika,
Mtaa wa Kuu,
S. L. P 201 Dodoma – Tanzania.
Simu: +255 26 232 2993.
Barua pepe: ushirika@ushika.go.tz



*Toleo la Kwanza*

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa andiko hili kwa namna yoyote ile, bila idhini ya Taasisi husika.

# YALIYOMO

YALIYOMO .......... ii

VIFUPISHO .......... iv

TAFSIRI ZA MANENO KAMA YALIVYOTUMIKA KATIKA MWONGOZO HUU .......... v

SURA YA KWANZA .......... 1

UTANGULIZI .......... 1

SURA YA PILI .......... 2

TARATIBU ZA UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA ZAO LA MIWA .......... 2

2.1 Usajili wa Mwanachama na Shamba la Miwa .......... 2

2.2 Usajili wa Vyama vya Ushirika wa Miwa .......... 2

2.3 Utaratibu wa Kulima na Usimamizi wa Mashamba ya Miwa .......... 2

2.4 Upatikanaji wa Wakandarasi katika Vyama vya Ushirika wa Miwa .......... 3

2.5 Kuvuna na Kuuza Miwa Kupitia Vyama vya Ushirika .......... 4

SURA YA TATU .......... 7

MAMBO YANAYOTAKIWA KUZINGATIWA NA TAASISI ZA FEDHA KATIKA UTOAJI MIKOPO KWA VYAMA VYA USHIRIKA VYA MIWA .......... 7

SURA YA NNE .......... 8

UANDAAJI NA UTOAJI WA TAARIFA .......... 8

4.1 Uandaaji wa Kumbukumbu na Vitabu vya Chama cha Ushirika .......... 8

4.2 Mfumo wa Uandaaji na Utoaji wa Takwimu .......... 9

SURA YA TANO .......... 10

WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU MBALIMBALI WA ZAO LA MIWA KATIKA MWONGOZO HUU .......... 10

5.1 Bodi ya Sukari Tanzania (Sugar Board of Tanzania - SBT) .......... 10

5.2 Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) .......... 11

5.3.1 Sekretarieti za Mikoa .......... 11

5.3.2 Mamlaka ya Serikali za Mitaa .......... 12

5.3 Wakala wa Vipimo .......... 12

5.4 Vyama Vya Ushirika Vya Miwa....12
5.5 kutoa taarifa mbalimbali kwa wadau wa usimamizi pindi zinapojitokeza au kuhitajika. Wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Wakulima wa Miwa....13
5.6 Mnunuzi....14
5.7 Taasisi za Fedha....15
5.8 Wakandarasi wa Uvunaji....15
5.9 Watoa Huduma za Kusambaza Pembejeo....16

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **DRD** | - | Daily Rate of Delivery |
| **GRN** | - | Goods Received Note |
| **SBT** | - | Sugar Board of Tanzania |
| **TCDC** | - | Tanzania Cooperative Development Commission |

## TAFSIRI ZA MANENO KAMA YALIVYOTUMIKA KATIKA MWONGOZO HUU.

| | | |
|---|---|---|
| **Ugavi** | - | Ni usambazaji wa huduma au bidhaa |
| **Ugani** | - | Ugani unahusisha utoaji maarifa, uzoefu na teknolojia inayohitajika kwa wanachama, ili kuongeza na kudumisha tija kwa ajili ya kuboresha ustawi na maisha ya wanachama na viwanda |
| **Usimamizi** | - | Mpango na uratibu wa shughuli za kibiashara kulingana na sheria ya Sukari Na. 26 ya mwaka 2001 na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 |
| **Wadau** | - | Wahusika wote katika tasnia ya sukari |
| **Uvunaji** | - | Inahusisha hatua zote za uchomaji, ukataji, upakiaji na usafirishaji wa miwa kutoka shambani kwenda kiwandani |
| **Mtoa huduma** | - | Mhusika yeyote kwenye mnyororo wa thamani wa zao la miwa |
| **Miwa** | - | Miwa inayotumika katika uzalishaji wa Sukari |
| **Mzabuni** | - | Mtu au Shirika linalouzia kampuni au Shirika lingine mahitaji yake kwa mikataba ya muda |
| **Mnunuzi** | - | Kiwanda cha Sukari |
| **Mkandarasi** | - | Ni mtoa huduma ya ukataji, upakiaji na usafirishaji wa miwa kwenda kiwandani |
| **Hati ya masafirisho ya bidhaa (*delivery note*)** | - | Ni hati iliyotolewa na msafirishaji wa bidhaa ikielezea bidhaa na idadi inayosafirishwa |
| **Tiketi za uzani (*weigh bridge tickets*)** | - | Ni hati za kisheria ambazo zinaonesha uzito, tarehe na wakati wa huduma. |
| **Hati ya kupokelea mzigo (*goods received note*)** | - | Hati inayotumika kuthibitisha bidhaa zote zilizopokelewa. Mara nyingi hulinganishwa na agizo la ununuzi kabla ya malipo kutolewa. |
| **Utoaji wa vocha za miwa** | - | Ni utoaji wa hati ya uhasibu inayowakilisha nia ya ndani ya |

| | |
|---|---|
| *(cane delivery voucher)* | malipo kwa chombo cha nje, kama vile muuzaji au mtoaji wa huduma, au vitabu vya kumbukumbu za mavuno ya miwa |

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ilitoa maelekezo, juu ya mfumo mpya wa uendeshaji wa biashara katika mazao ya kimkakati, kufanyika kupitia Mfumo wa Vyama vya Ushirika. Aidha, miongoni mwa mazao yaliyotolewa maelekezo na Serikali ni pamoja na zao la miwa ya sukari, linalolimwa katika maeneo mbalimbali nchini. Lengo la Serikali kuweka mfumo huo mpya wa kiuendeshaji, ni kutaka kuhakikisha kuwa, kilimo cha miwa kinamnufaisha mwanachama sanjari na kuondoa mfumo holela wa uendeshaji wa zao hilo, ambao kimsingi ulikuwa hauna tija kwa mwanachama. Aidha, biashara ya miwa ya sukari inasimamiwa na sheria mbili kwa karibu, ambazo ni Sheria ya Tasnia ya Sukari namba 26 ya mwaka 2001 pamoja na kanuni zake za mwaka 2010, na Sheria ya Vyama vya Ushirika namba 6 ya mwaka 2013 pamoja na kanuni zake za mwaka 2015.

Hivyo basi, kwa kuzingatia hayo, Bodi ya Sukari Tanzania na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, kama wasimamizi wakuu wa masuala ya biashara ya miwa ya sukari na kwa kushirikisha wadau wa Tasnia ya Sukari nchini, wameandaa mwongozo wa usimamizi wa biashara ya zao la miwa ya sukari na usimamizi wa Tasnia hiyo kwa ujumla.

Lengo kuu la mwongozo huu, ni kutoa utaratibu kwa wadau wa miwa nchini, katika kusimamia na kuratibu shughuli za uendeshaji wa biashara ya miwa ya sukari ambazo ni pamoja na kuainisha taratibu za uendeshaji na usimamizi wa zao la miwa, kuainisha mambo yanayotakiwa kuzingatiwa na taasisi za fedha katika utoaji mikopo kwa Vyama vya Ushirika vya Miwa, kuweka taratibu za uandaaji na utoaji wa taarifa na kuainisha wajibu na majukumu ya wadau mbalimbali wa zao la miwa. Hii ni kwa kuzingatiakuwa, pamekuwa na uendeshaji holela wa zao la miwa ya sukari kinyume na malengo ya serikali na matarajio ya wanachama. Aidha, ni matarajio ya wadau wote wa usimamizi, pamoja na serikali kuwa, mwongozo huu utazingatiwa na kutekelezwa wakati wa kuendesha na kusimamia biashara ya miwa katika Tasnia ya sukari nchini.

## SURA YA PILI

## TARATIBU ZA UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA ZAO LA MIWA

### 2.1 Usajili wa Mwanachama na Shamba la Miwa

Kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya Sukari ya mwaka 2001 pamoja na kanuni zake za mwaka 2010, inaelekeza kila mwanachama wa miwa na shamba/mashamba, asajiliwe na kutambuliwa na Bodi ya Sukari Tanzania. Kwa kuzingatia hilo, kila mwanachama atasajiliwa kwanza, kabla ya kuandikishwa kuwa mwanachama wa chama cha ushirika katika eneo husika, kama inavyoelekeza katika Sheria ya Vyama vya Ushirika namba 6 ya mwaka 2013 na Kanuni zake za mwaka 2015. Aidha, wanachama/mwanachama mwenye mashamba ya miwa yaliyotawanyika katika maeneo yanayohudumiwa na vyama vya ushirika tofauti, kwa idhini ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika, anaweza kumruhusu mwanachama husika kuwa na uanachama katika kila chama husika, endapo atajiridhisha kwa kuzingatia sheria, kanuni na utaratibu uliopo.

### 2.2 Usajili wa Vyama vya Ushirika wa Miwa

Vyama vya Ushirika vya Wanachama wa Miwa vitasajiliwa kwa mujibu Sheria ya Vyama vya Ushirika namba 6 ya mwaka 2013 na Kanuni zake za mwaka 2015. Aidha, katika usajili wa vyama hivi mambo yafuatayo yatazingatiwa;

(i) Taarifa ya usajili wa wanachama wa miwa na mashamba yao kutoka Bodi ya Sukari Tanzania;

(ii) Uwepo wa chama kimoja cha ushirika wa miwa katika eneo moja la kijiografia litakaloainishwa katika maombi ya usajili; na;

(iii) Mambo mengine kama itakavyoonekana inafaa katika utekelezaji wa shughuli zihusuzo Biashara ya miwa, kupitia vyama vya Ushirika.

### 2.3 Utaratibu wa Kulima na Usimamizi wa Mashamba ya Miwa

Kilimo cha zao la miwa kinaendeshwa kwa kuzingatia kanuni na taratibu za kilimo bora kama zilivyoainishwa katika Kanuni za Sheria ya Tasnia ya Sukari za mwaka 2010. Kanuni hizo zinaelekeza mwanachama wa miwa kuzingatia mambo yafuatayo: -

(i) Mwanachama wa miwa haruhusiwi kupanda jamii za miwa ambazo hazijaidhinishwa na Mamlaka zinazohusika na mbegu;

(ii) Haruhusiwi kuhamisha miwa kutoka shamba moja kwenda lingine pasipokuwa na kibali kutoka katika Mamlaka husika;

(iii) Haruhusiwi kupanda miwa ambayo kitaalamu ina viashiria vya magonjwa ya miwa;

(iv) Anapaswa kutunza shamba na kuweka mikuza itakayokabiliana na moto wakati wa uvunaji, na ajali za moto zisizotarajiwa; na;

(v) Anapaswa kulima kilimo kinachozingatia kanuni na taratibu za Utunzaji waMazingira.

### 2.4 Upatikanaji wa Wakandarasi katika Vyama vya Ushirika wa Miwa

Vyama vya Ushirika wa Miwa huendesha shughuli zao kwa kutoa zabuni kwa wakandarasi wa uvunaji wa miwa. Kwa mujibu wa mwongozo huu vyama vya ushirika vya wanachama wa miwa vitapaswa kuzingatia Mwongozo wa Manunuzi wa Vyama vya Ushirika katika mchakato wa kuwapata wakandarasi pamoja na kuzingatia vigezo vifuatavyo: -

(i) Kwa chama ambacho kina kiwango cha kuingiza miwa kiwandani kwa siku (DRD), chini ya Tani 200, hakipaswi kutoa zabuni kwa mkandarasi zaidi ya mmoja;

(ii) Chama kinawajibika kufanya upekuzi wa vitendea kazi vya wakandarasi na kutoa taarifa ya upekuzi huo na kuiwasilisha kwa Mrajis (Ofisi ya Ushirika) kabla ya kutoa zabuni;

(iii) Mikataba ya ukandarasi iainishe vigezo vya ufanisi wa utoaji huduma za uvunaji miwa vitakavyolinda ubora wa miwa na shamba, kupunguza upotevu na kuhakikisha usalama wa watu na mali;

(iv) Mikataba ya ukandarasi wa uvunaji wa miwa itadumu kwa kipindi kisichopungua miaka miwili (2) na kisichozidi miaka mitatu (3);

(v) Mikataba ya ukandarasi itatakiwa kuwasilishwa na Chama cha Ushirika kwa Mrajiswa Vyama vya Ushirika kwa ajili ya upekuzi (*vetting*) kabla ya kusainiwa;

(vi) Mikataba iainishe kipengele cha kufanya mapitio ya utendaji kazi wa mkandarasi kila baada ya miezi mitatu (3), kwa ajili ya kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake; na

(vii) Mikataba iainishe kipengele cha kufanya mapitio kwenye mikataba hiyo kila mwaka kwa ajili ya kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wakandarasi.

## 2.5 Kuvuna na Kuuza Miwa Kupitia Vyama vya Ushirika

Jukumu kubwa la Vyama vya Ushirika ni shughuli za kuvuna na kuuza miwa, ambazo zinabeba dhima kubwa ya biashara ya miwa ya sukari. Kwa kuzingatia hili, mwongozo huu unaelekeza kwa kina namna ya kuendesha shughuli hizo kama ifuatavyo:

### i) Kalenda ya Masoko ya Zao la Miwa

Kulingana na kuanza na kumalizika kwa msimu wa masoko wa zao la miwa katika viwanda vya sukari Tanzania Bara, mwongozo huu, unaelekeza kuwa, shughuli za masoko katika zao la miwa zitaanza rasmi *tarehe 01 mwezi Mei, na kumalizika tarehe 30 mwezi Apili mwaka unao fuata* .

### ii) Uandaaji wa Ratiba za Uvunaji

Kutokana na kutokuwepo na uhuru wa mwanachama kuvuna wakati wowote, Chama cha Ushirika kitawajibika kuwa na ratiba ya uvunaji. Ratiba za uvunaji hizo katika Vyama vya Ushirika vya wanachama wa miwa, zitaandaliwa na Vyama vya Ushirika vyenyewe kwa kuzingatia misingi ya uwazi, kanuni bora za kilimo cha miwa na kwa kuwashirikisha wanachama kupitia Mikutano Mikuu. Aidha, endapo zitatokea sababu za msingi zitakazolazimu ratiba za uvunaji kubadilika, ni lazima Bodi ya Uongozi wa chama husika ikubaliane kupitia vikao vyake, na mwishoni mwa msimu wanachama wapatiwe taarifa ya utekelezaji wa ratiba za uvunaji kupitia Mkutano Mkuu.

### iii) Uuzaji wa Miwa ya Sukari

Kwa kuzingatia Sheria ya Tasnia ya Sukari namba 26 ya Mwaka 2001 na kanuni zake za mwaka 2010, kiwanda kitanunua miwa kwa mwanachama wa chama cha Ushirika cha miwa, aliyesajiliwa na Bodi ya Sukari Tanzania kupitia chama cha ushirika. Aidha, Bodi ya Sukari Tanzania hufanya usajili wa wanachama wa miwa na mashamba ya miwa na kutoa namba za

utambulisho kwa kila mwanachama pamoja na shamba husika. Namba ya shamba inapaswa kuwa namba ya kuvunia, ambapo itaweka udhibiti wa kila shamba kuvunwa kwa namba yake. Mwanachama mwenye mashamba mengi atapata namba ya kuvunia kwa kila shamba. Ili kusimamia shughuli hii ya uuzaji kikamilifu utaratibu ufuatao utafuatwa: -

(i) Bodi ya Sukari itatoa namba za usajili wa wanachama na mashamba na kukipatia chama cha ushirika orodha hiyo;
(ii) Kila mwanachama wa miwa atapaswa kuwa na akaunti ya benki itakayokuwa inafanyiwa malipo ya uuzaji wa miwa, na atapaswa kuwasilisha taarifa stahiki za akaunti hiyo kwa chama cha ushirika;
(iii) Chama cha Ushirika kitahakikisha wanachama wake wote wamesajiliwa, na kitawasilisha namba za wanachama na mashamba yao kwa kiwanda cha Sukari, pamoja na akaunti zao za benki zitakazopokea malipo ya miwa; na
(iv) Kiwanda cha Sukari kitatoa namba za kuuzia miwa kwa kila mwanachama aliyesajiliwa na kutumia namba za mashamba kama namba za kuvunia.

**iv) Udhibiti wa Moto wa Makusudi (*Malicious Fire*)**

Mara nyingi uvunaji wa miwa huwa unafanyika kwa kuchoma moto shamba la miwa, ndipo shughuli za uvunaji zifanyike. Pamekuwa na uchomaji wa mashamba kwa makusudi, nje ya utaratibu ili kushinikiza kuvuna miwa, ambapo ni kinyume na Kanuni za Sheria ya Tasnia ya Sukari ya Mwaka 2010. Hivyo basi, mwongozo huu unaelekeza vyama vya ushirika kushirikiana na mamlaka za serikali za vijiji kuimarisha ulinzi wa mashamba ya miwa yaliyo katika maeneo yao, ili kudhibiti moto wa makusudi pamoja na ajali nyinginezo za moto, katika mashamba ya miwa.

**v) Kuingia Mikataba ya Ugavi wa Miwa kati ya Vyama vya Ushirika na Kiwanda.**

Kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya Sukari Na.26 ya mwaka 2001 na Kanuni zake za mwaka 2010, zinaelekeza chama cha ushirika cha wanachama wa miwa kuingia katika mikataba ya ugavi wa miwa (*Cane Supply Agreement*) na Kiwanda cha miwa, kwa lengo la kuchakata miwa ya Sukari. Aidha, mikataba hiyo itazingatia mambo mbalimbali yenye lengo la kumnufaisha mwanachama na viwanda, na pia kufanikisha utekelezwaji wa mikataba hiyo kama ifuatavyo: -

(i) Kiwango cha miwa kitakachopelekwa na Chama cha Ushirika kiwandani;

(ii) Majukumu ya kiwanda na ya mwanachama kuhusiana na uvunaji na usafirishaji wa miwa mpaka kiwandani;

(iii) Ratiba ya uvunaji na uwasilishaji wa miwa kiwandani;

(iv) Kiasi cha malipo kitakacholipwa na kiwanda kwa mwanachama kwa kila tani moja ya miwa;

(v) Masharti ya malipo yatakayozingatiwa na kiwanda kabla ya kufanya malipo kwa mwanachama; na;

(vi) Muda wa kufanya malipo kwa mwanachama wa miwa.

## SURA YA TATU

## MAMBO YANAYOTAKIWA KUZINGATIWA NA TAASISI ZA FEDHA KATIKA UTOAJI MIKOPO KWA VYAMA VYA USHIRIKA VYA MIWA

Pamoja na taratibu zilizoainishwa katika Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika, taasisi za kifedha, pamoja na mambo mengine, zina wajibu wa kuzingatia mambo yafuatayo wakati wa utoaji wa mikopo kwenye Vyama vya Ushirika vya wanachama wa miwa:

(i) Mahitaji halisi ya pembejeo kwa mwanachama mmoja mmoja, sambamba na makadario ya bajeti ya pembejeo yaliyoidhinishwa na Mrajis;

(ii) Dhamana ya mwanachama au Chama cha Ushirika husika, ikizingatia thamani halisi ya mkopo unaoombwa kwa ajili ya pembejeo;

(iii) Namba ya utambulisho wa mwanachama wa nje (*SBT Outgrower Number*);

(iv) Ratiba za uvunaji za Vyama Vya Ushirika;

(v) Taarifa za ukaguzi wa fedha za chama; na

(vi) Hati ya Ukomo wa madeni unaotolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

## SURA YA NNE

## UANDAAJI NA UTOAJI WA TAARIFA

### 4.1 Uandaaji wa Kumbukumbu na Vitabu vya Chama cha Ushirika

Vyama vya Ushirika vinapaswa kutunza kumbukumbu muhimu za miamala yote inayohusika na wanachama wa zao la miwa, katika mnyororo mzima wa thamani, pamoja na kumbukumbu za malipo kwa wanachama wote. Hivyo, Chama cha Ushirika kitakuwa na wajibu wa kutumia vitabu vifuatavyo: -

(i) Vitabu vya mapokezi ya pembejeo kutoka kwa wasambazaji yaani *"Goods Received Note (GRN)"* ili kuonesha jina la msambazaji wa pembejeo, aina ya pembejeo, kiasi na lini pembejeo zilipokelewa chamani toka kwa mzabuni aliyeidhinishwa;

(ii) Vitabu vya ugawaji wa pembejeo *(Delivery note)* kwa wanachama, kwa kuzingatia mahitaji halisi yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu na kuidhinishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika;

(iii) Vitabu vya kumbukumbu za mavuno na usafirishaji wa miwa ya wanachama (*Cane delivery Note*) kwa kuzingatia muda wa gari kuondoka shambani, tarehe ya mavuno, jina la mwanachama, namba ya gari, namba ya utambulisho wa gari, namba ya usajili wa mwanachama, na mkandarasi aliyevuna na kupakia miwa;

(iv) Vitabu vya kumbukumbu za mapokezi ya miwa *(Weigh bridge ticket)*, ikionyesha namba ya gari, namba ya utambulisho wa gari, jina la mwanachama, namba ya usajili wa mwanachama, umbali wa miwa ilipotoka, namba ya stakabadhi ya usafirishaji *(cane delivery note),* tarehe ya kuchoma na kuvuna miwa, tarehe ya mapokezi kwenye mizani na uzito wa miwa.

(v) Nakala za kumbukumbu za mauzo (*Cane payment Voucher*) ya miwa kwa mnunuzi, kwa kuzingatia kiasi cha miwa kilichowasilishwa, kiwango cha sukari kilichobainika na thamani yake, makato halali pamoja na kiasi halisi kitakacholipwa kwa mwanachama kupitia akaunti yake ya Benki. Aidha, mwanachama anapaswa kupokea vocha yake ya kumbukumbu ya malipo kupitia chama chake cha msingi.

(vi) Hati za malipo, stakabadhi ya fedha, daftari za fedha, leja kuu na vitabu vya masawazisho (*Journal*), daftari la mali za kudumu na daftari la wanachama.

### 4.2 Mfumo wa Uandaaji na Utoaji wa Takwimu

Kutakuwa na mfumo sahihi wa uandaaji na utoaji wa takwimu za wanachama wa zao la miwa. Takwimu hizo zitapaswa kutunzwa kwa kuzingatia yafuatayo: -

(i) Chama cha Ushirika kitatakiwa kutunza kumbukumbu za wanachama wake kwa mfumo wa nakala laini na ngumu (*Soft and Hard copies*) kwa kuzingatia jina la mwanachama, namba ya mwanachama, ekari anazolima, uzito wa mavuno, kiasi cha malipo, aina na kiasi cha mapato kilichopatikana; na

(ii) Taarifa za kumbukumbu za wanachama zitawasilishwa kila baada ya kipindi cha robo mwaka kwa wadau mbalimbali wanaohusika, kupitia kwa maafisa ushirika wa eneo husika.

## SURA YA TANO

## WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU MBALIMBALI WA ZAO LA MIWA KATIKA MWONGOZO HUU

### 5.1 Bodi ya Sukari Tanzania *(Sugar Board of Tanzania - SBT)*

(i) Kukuza maendeleo na upanuzi wa kilimo cha miwa, uzalishaji na soko la sukari na bidhaa nyingine zitokanazo na miwa;

(ii) Kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika na wadau wengine wa Tasnia ya sukari kuandaa jukwaa la wanachama kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali yahusuyo kilimo cha miwa;

(iii)Kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kufanya mapitio, maboresho na kusajili mikataba ya ugavi na ununuzi wa miwa (*Cane Supply Agreement*);

(iv)Kutoa mafunzo kwa wanachama wa miwa na kusimamia utekelezaji wa mbinu bora za kuzuia magonjwa na wadudu wa miwa;

(v) Kuweka mazingira bora ya ushindani wa kibiashara kati ya wadau wa Tasnia ya sukari;

(vi)Kutoa maelekezo, miongozo na kusimamia namna bora ya kulima miwa na matumizi ya mbegu bora;

(vii) Kuteua wasimamizi na wakaguzi wa mashamba ya miwa, mitambo ya sukari, mabohari ya sukari na vifaa vyovyote ambavyo vinaweza kukaguliwa kwa dhumuni la utekelezaji bora wa mwongozo huu;

*(viii)* Kukuza, kuendeleza na kuwezesha uanzishwaji wa vyama vya ushirika au vikundi vingine vya wadau katika Tasnia ya sukari (ambavyo vitakuwa jukwaa la ushauri kwa Bodi) na kusimamia utendaji wake wa kazi ilimradi vyama hivyo visijihusishe na upangaji wa bei ya sukari au kufanya kitu chochote ambacho ni kinyume na Sheria ya Ushindani wa Biashara *(Fair Competition Act, 1994);*

(ix) Kusimamia utekelezaji wa mipango ya upanuzi wa viwanda vya uzalishaji wa sukari;

(x) Kukusanya, kuboresha, kutunza na kusambaza takwimu na taarifa zinazohusiana na kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari; na

(xi)Kutekeleza majukumu mengine kadiri yatakavyokuwa yakijitokeza, kwa kushirikiana na wadau wengine wa Tasnia ya Sukari.

5.2 **Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)**

(i) Kuratibu na kusimamia mchakato wa vyama vya ushirika vya miwa, katika kupata viongozi wa chama;

(ii) Kuhamasisha wakulima katika maeneo yanayolima zao la miwa kuanzisha na kujiunga na vyama vya ushirika kulingana na mahitaji;

(iii) Kusajili au kufuta vyama vya ushirika vya miwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika pamoja na kanuni zake;

(iv) Kushiriki katika majadiliano ya mikataba ya ununuzi na ugavi wa miwa (*Cane Supply Agreement)* na kutoa idhini kabla ya mikataba kusainiwa;

(v) Kusimamia na kuhakikisha wanachama wote wa miwa wanalipwa kikamilifu na kwa wakati, kulingana na mkataba uliosainiwa ;

(vi) Kufanya usimamizi na udhibiti juu ya uendeshaji wa biashara ya zao la miwa, kwa mujibu wa mfumo wa Vyama vya Ushirika;

(vii) Kufanya ukaguzi, usimamizi na udhibiti wa Vyama vya Ushirika vya miwa;

(viii) Kutoa mafunzo na elimu kwa wanachama na viongozi kuhusiana na namna bora ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika;

(ix) Kuratibu vikao baina ya Vyama vya Ushirika na wadau wengine katika maeneo husika, kwa ajili ya kujadili gharama za ukataji, upakiaji na usafirishaji wa miwa kabla ya msimu kuanza;

(x) Kufanya utatuzi wa migogoro inayojitokeza kwenye Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia sheria ya vyama vya ushirika pamoja na kanuni zake;

(xi) Kufanya tathmini ya shughuli za kilimo cha miwa kila msimu, kwa kushirikiana na Bodi ya Sukari Tanzania na wadau wengine wa usimamizi katika Tasnia ya Sukari na;

(xii) Kusimamia Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba 6 ya mwaka 2013 na Kanuni zake za mwaka 2015 wakati wote wa uendeshaji wa Vyama vya Ushirika wa miwa.

5.3.1 **Sekretarieti za Mikoa**

Kuratibu maendeleo ya zao la miwa ya sukari kupitia mfumo wa ushirika kwa kushirikiana na wadau wengine wa usimamizi.

### 5.3.2 Mamlaka ya Serikali za Mitaa

(i) Kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika kusimamia utendaji wa Vyama vya Ushirika vya zao la miwa;

(ii) Kuhamasisha uanzishwaji na uandikishwaji wa Vyama vya Ushirika vya miwa katika maeneo yao, kulingana na mahitaji;

(iii) Kuratibu na kusimamia ulipwaji wa madeni ya wanachama wa zao la miwa kutoka kwa wanunuzi, kupitia mfumo wa uendeshaji wa Vyama vya Ushirika;

(iv) Kusimamia makusanyo ya mapato ya serikali yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria;

(v) Kutoa mafunzo na elimu kwa wanachama, kuhusiana na namna ya kuendesha shughuli za uzalishaji na uuzaji wa miwa kwa mujibu wamfumo wa ushirika;

(vi) Kusimamia shughuli za ugani katika zao la miwa;

(vii) Kushirikiana na vyama vya ushirika katika kukarabati miundombinu;' na

(viii) Kushughulikia kwa ufanisi mambo mengine yatakayojitokeza, kwa kushirikiana na wadau wengine wa usimamizi wa zao la miwa.

### 5.3 Wakala wa Vipimo

(i) Kukagua na kupitisha mizani ya kupimia miwa kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria;

(ii) Kutoa mafunzo ya matumizi sahihi ya mizani;

(iii) Kufanya ukaguzi wa mizani, wa kupanga na wa kushtukiza wakati msimu wa ununuzi ukiendelea; na

(iv) Kushirikiana na wadau wa Tasnia ya Sukari kutatua migogoro itokanayo na vipimo.

### 5.4 Vyama Vya Ushirika Vya Miwa

(i) Kuchagua viongozi wenye sifa stahiki na uadilifu, katika kusimamia shughuli na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika vya miwa;

(ii) Kuajiri watendaji wenye sifa na vigezo stahiki, chini ya usimamizi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika;

(iii) Kuhakikisha kila mwanachama ni mkulima wa miwa na amesajiliwa na Bodi ya Sukari Tanzania;

(iv) Kuwaajiri kwa muda na kuwasimamia wakandarasi, ili kuhakikisha wanakidhi vigezo vya ufanisi vilivyoainishwa kwenye mikataba na kuchukua hatua stahiki pale inapolazimu ;

(v) Kusimamia malipo ya wakulima wa miwa pamoja na makato ya serikali, kwa kuzingatia mjengeko wa bei ulioidhinishwa na kukubaliwa na wadau;

(vi) Kuhakikisha miundombinu ya mashambani inakarabatiwa na kuwa katika hali nzuri wakati wote wa shughuli za kilimo cha miwa;

(vii) Kufanya ufuatiliaji na kuhakikisha mikopo yote iliyochukuliwa na chama au wanachama, kwa shughuli za kilimo, inarejeshwa kwa wakati uliopangwa;

(viii) Kupanga na kuratibu ratiba ya uvunaji wa miwa na kusimamia uendeshwaji wa biashara ya zao la miwa kwa kushirikiana na wadau wa usimamizi;

(ix) Kutunza kwa usahihi takwimu za ununuzi wa miwa kutoka kwa wanachama na kutoa taarifa sahihi kwa wadau wengine wa usimamizi pindi zinapohitajika;

(x) Kuhakikisha kila mwanachama anafungua akaunti kwa ajili ya malipo ya miwa;

(xi) Kufanya majadiliano ya mikataba ya kupanga bei ya zao la miwa (*Cane Supply Agreement*) na mnunuzi/wanunuzi kwa kushirikisha wadau wa usimamizi wa Tasnia ya Sukari;

(xii) Kuwasilisha mikataba ya ununuzi na ugavi wa miwa katika ofisi ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa ajili ya upekuzi (*Vetting*) kabla ya kusainiwa;

(xiii) Kuingia mikataba baina ya vyama na mnunuzi/wanunuzi kwa kushirikiana na wadau wa usimamizi;

(xiv) Kuandaa sera ya usimamizi wa mifuko ya maendeleo ya chama;

(xv) Kusimamia na kuhakikisha ubora wa zao la miwa;

(xvi) Kuhakikisha wanachama wanapata elimu bora ya kilimo cha miwa;

(xvii) Kushirikiana na wadau wengine wa usimamizi katika Tasnia ya Sukari; na

***kutoa taarifa mbalimbali kwa wadau wa usimamizi pindi zinapojitokeza au kuhitajika.***

### 5.5 Wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Wakulima wa Miwa

(i) Kutunza miwa kwa kuzingatia vigezo na masharti ya kilimo bora kama yatakavyokuwa yakitolewa na Bodi ya Sukari nchini;

(ii) Kutoa taarifa na kuomba idhini ya kupanua au kuongeza mashamba ya miwa, kutoka Bodi ya Sukari Tanzania, kupitia chama chake cha Ushirika;

### 5.9 Watoa Huduma za Kusambaza Pembejeo

Vyama vya Ushirika vya wakulima wa Miwa vina wajibu wa kuhakikisha wanachama wao wanapatiwa pembejeo zenye ubora na kwa bei nafuu. Katika kutekeleza wajibu huo chama kitaagiza pembejeo moja kwa moja kutoka kwa wasambazaji wakuu wa pembejeo nchini au kitatumia mzabuni (***atakayepatikana kwa mujibu wa mwongozo wa manunuzi wa Vyama vya Ushirika***) atakayekuwa na wajibu wa kusambaza pembejeo kwenye Chama cha Ushirika.

Mwongozo huu umesainiwa na:

DIRECTOR GENERAL
SUGAR BOARD OF TANZANIA
SUKARI HOUSE
CORNER OF OHIO/SOKOINE DRIVE
P. O. Box 4355
DAR ES SALAAM

| | |
|---|---|
| Prof. Kenneth Bengesi | Dkt. Benson O. Ndiege |
| **Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Miwa Tanzania** | **Mrajis wa Vyama vya Ushirika Tanzania** |
| Tarehe: 22 March 2022 | Tarehe: 23/02/2022 |